

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA
UPIMAJI WA KITAIFA WA DARASA LA NNE**

05

SAYANSI NA TEKNOLOJIA

Muda Saa 1:30

Mwaka: 2021

Maelekezo

1. Karatasi hii ina sehemu A na B zenye jumla ya maswali **matano (5)**
2. Jibu maswali yote katika kila sehemu.

SEHEMU A (Alama 30)

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii

1. Jibu vipengele (i) na (v) kwa kuchagua herufi ya jibu sahihi na kuiandika kwenye kisanduku.
 - (i) Nini kazi ya antenna katika redio?
A. Kurekebisha sauti
B. Kuchukua mawimbi angani
C. Kurekebisha stesheni
D. Kupaza sauti []
 - (ii) Ni vifaa vipi vya kisasa hutumika katika mawasiliano?
A. Simu, redio na runinga
B. Ngoma, filimbi na runinga
C. Raedio, gazeti na baragumu
D. Simu, ngoma na baragumu []
 - (iii) Ni kwa namna gani mawasiliano ya picha na maandishi huoneshwa katika runinga?
A. Kupitia spika
B. Kupitia skrini
C. Kupitia antena
D. Kupitia rimoti []
 - (iv) Ni kampuni ipi **haitoi** huduma za mitandao ya simu Tanzania?
A. TTCL
B. VODACOM
C. TECNO
D. TIGO []
 - (v) Simu zinazopigwa unapohitajika msaada wa haraka zinaitwaje?
A. Simu za upepo
B. Simu muhimu
C. Simu za sauti
D. Simu za dharura []
2. Jibu vipengele (i) hadi (v) kwa kuoanisha dalili za magonjwa katika **Orodha A** na magonjwa husika katika **Orodha B**. andika herufi ya jibu sahihi kwenye mabano.

	Kundi A	Majibu	Kundi
(i)	Kukakamaa viungo na kupinda shingo	[]	A. Kifua
(ii)	Kuota vipele vidogo vidogo Mwilini	[]	B. Kisukari
(iii)	Kujisaidia kinyesi kama maji yaliyooshea mchele	[]	C. Pepopunda D. Kuhara
(iv)	Kukojoa mara kwa mara	[]	E. Surua
(v)	Kutoa sauti kama filimbi wakati wa kupumua.	[]	F. Pumua G. Kipindupindu

3. Jibu vipengele (a) hadi (e) kwa kuandika hatua za uchunguzi wa kisayansi zilizo katika kisanduku.

Kuchambua data, jaribio,	Kutafsiri matokeo, Kubainisha tatizo.	Kubuni dhanio,	Kufanya
-----------------------------	------------------------------------------	----------------	---------

- (a) Hatua ya kwanza _____
(b) Hatua ya pili _____
(c) Hatua ya tatu _____
(d) Hatua ya nne _____
(e) Hatua ya tano _____

SEHEMU B (Alama 20)

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii


4. Soma kifungu cha habari kifuatacho, kisha jibu vipengele (a) hadi (e) kwa kuandika jibu sahihi katika nafasi zilizoachwa wazi.

Uvaaji wa nguo chafu husababisha harufu mbaya mwilini na wakati mwingine magonjwa ya ngozi. Nguo safi humfanya mtu kuonekana nadhifu na wa kuvutia. Ili kufanya nguo ziwe safi, ni lazima zifuliwe kwa kutumia maji safi na sabuni. Baada ya nguo kukauka zinapaswa kupigwa pasi ili kua vimelea vya magonjwa. Pia upigaji nguo pasi unamfanya mvaaji aonekane nadhifu. Nguo zikishakuwa safi zinaweza kuvaliwa au kuhifadhiwa sehemu safi na kavu, kama vile sandukuni au kabatini.

Maswali:

- (a) Ni vifaa gani vinahitajika wakati wa ufuaji nguo?
(i) _____ (ii) _____
- (b) Athari ya kuvaa nguo chafu ni nini?
- (c) Kwanini tunapiga nguo pasi? Toa sababu moja _____
- (d) Nini kinaua vimelea wakati wa kupiga pasi? _____
- (e) Kwa nini nguo safi huhifadhiwa kabatini au sandukuni? _____

5. Tumia vifaa vilivyooneshwa katika picha kujibu kipengele (a) hdi (e). Andika jibu katika nafasi uliyopewa.



- (a) Kifaa kipi kinatoa kipimo kisicho rasmi?
- (b) Kifaa kipi hupima ujazo wa maji kwa usahihi?
- (c) Urefu wa dawati hupimwa kwa kifaa kipi?
- (d) Kifaa kipi hutumika kupima uzito wa kitu?
- (e) Kwa nini kipimo kilichopimwa na ruala ni kipimo rasmi?